**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**Anwani ya Simu : "TUME"**
**DODOMA**
**Nambari ya Simu:** 0738 166703
0733 005974
**Barua pepe:** Secretary@psc.go.tz
**Tovuti:** *www.psc.go.tz*

Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga (UDOM),
Ghorofa ya 2,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
**40405 DODOMA.**

# TAARIFA KWA UMMA

## MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA – TANZANIA (PSC), JAJI (Mst) HAMISA H. KALOMBOLA AMECHAGULIWA KUWA MAKAMU WA RAIS WA JUMUIYA YA TUME ZA UTUMISHI WA UMMA AFRIKA (AAPSCOMs) KANDA YA AFRIKA MASHARIKI

Mkutano Mkuu wa 6 wa Jumuiya ya Tume za Utumishi wa Umma Afrika (AAPSCOMs) uliofanyika Jijini Nairobi umemchagua Mhe. Jaji (Mst) Hamisa H. Kalombola ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma – Tanzania (PSC) kuwa Makamu wa Rais wa Jumuiya ya Tume za Utumishi wa Umma Afrika (AAPSCOMs) Kanda ya Afrika Mashariki katika kikao kilichofanyika kuanzia tarehe 6 hadi 8 Novemba, 2024 katika Ukumbi wa Hoteli ya Safari Park.

Mkutano huo uliandaliwa na Serikali ya Kenya kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya hiyo na Tume ya Utumishi wa Umma ya Kenya na mgeni rasmi katika hafla ya ufunguzi alikuwa Mhe. Justin B.N. Muturi - Waziri wa Utumishi wa Umma na Maendeleo ya Rasilimali Watu, Kenya.

Mkutano huo uliandamana na Maadhimisho ya Miaka 16 ya Jumuiya hiyo iliyoanzishwa mwaka 2008 kama chombo cha kubadilishana uzoefu, kushirikiana, kuweka malengo ya pamoja na kujadiliana kuhusu changamoto mbalimbali zinazoukabili Utumishi wa Umma Afrika.

Kauli Mbiu ya Mkutano huo ilikuwa "**KUCHOCHEA MABADILIKO KATIKA UTUMISHI WA UMMA KUPITIA UBUNIFU NA MAENDELEO YA TEKNOLOJIA**."
**(Driving Public Service delivery Transformation through Innovation and Technology)**

Pamoja na majadiliano mbalimbali yaliyofanyika kuhusu maendeleo ya Sekta ya Utumishi wa Umma katika Bara la Afrika, wajumbe wa mkutano huo walifanya uchaguzi wa viongozi ambao muda wao ulikuwa umekwisha. Viongozi waliochaguliwa katika Mkutano huo na Wenyeviti wa Tume kutoka Kanda mbalimbali zilizo ndani ya Jumuiya hiyo ni kama ifuatavyo:

i. Mhe. Balozi Anthony M. Muchiri CBS – Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma ya Kenya amechaguliwa kuwa Rais wa Jumuiya ya Tume za Utumishi Afrika (AAPSCOMs).

ii. Mhe. Jaji (Mst) Hamisa H. Kalombola – Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Tanzania amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais - Kanda ya Afrika Mashariki (AAPSCOMs).
iii. Mhe. Prof. Somadoda Fikeni - Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma Afrika Kusini amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais - Kanda ya Kusini Mwa Afrika (SADC).
iv. Mhe. Prof. Tunji Olaopa – Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Nigeria amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais - Kanda ya Afrika Magharibi (AAPSCOMs).

Mkutano huo umehudhuriwa na nchi 10 za Afrika ikiwemo Tanzania, Zambia, Afrika Kusini, Ufalme wa Lesotho, Nigeria, Gambia, Namibia, Zimbabwe, Ufalme wa Eswatini na Kenya ambapo jumla ya Taasisi zilizoshiriki zilikuwa 26.

Mkutano Mkuu wa 7 wa Jumuiya ya Tume za Utumishi wa Umma Afrika (AAPSCOMs) unatarajiwa kufanyika nchini Nigeria, Kanda ya Afrika Magharibi kulingana na Kalenda ya Jumuiya hiyo.

Imetolewa na:

Bw. Mathew M. Kirama
**KATIBU**
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA (PSC)**
25 Novemba, 2024